TANGAZO LA SERIKALI Na. 217 la tarehe 15/4/2022

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

Zimetungwa chini ya Kifungu cha 7 (1) na 16(1)

SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU YA HALMASHAURI YA WILAYA YA IKUNGI, 2022

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi ya Mwaka 2022.

Tafsiri

2. Katika Sheria Ndogo hii isipokuwa kama muktadha utaeleza vinginevyo;

"ada" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya vibali au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi;

"gari" maana yake ni chombo chochote kinachotumika kusafirisha abiria au mizigo kutoka sehemu moja kwenda nyingine na chenye leseni ya kufanya shughuli hiyo.

"kibali cha ujenzi" maana yake ni kibali kinachotolewa na Halmashauri kwa ajili ya ujenzi ambao unafanyika ndani ya eneo la Mamlaka ya Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii au Kanuni na Sheria zinazosimamia ujenzi;

"maegesho" maana yake ni sehemu au eneo lililotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuegesha magari au vyombo vya usafiri au vyombo vya moto;

"mazao" maana yake ni mazao yote yatokanayo na shughuli za mashambani ikijumuisha mazao ya chakula, biashara pamoja na mazao ya misitu;

"matangazo" maana yake ni matangazo yanayotangazwa kwa kutumia vipaza sauti kwa ajili ya kutangaza biashara ya aina yeyote katika eneo la Halmashauri ikijumuisha matangazo katika masoko, magulio, sherehe, mikutano isipokuwa matangazo ya vifo au misiba;

Sura ya 323

"mazao ya misitu" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika kifungu cha 2 cha Sheria ya Misitu,

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi pamoja na Afisa yeyote atakayeteuliwa kufanya kazi za Mkurugenzi kwa wakati huo;

"ushuru" maana yake ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa shughuli au huduma mbalimbali zinazofanywa katika eneo la Halmashauri;

"ushuru wa soko" maana yake ni ushuru ambao hutozwa kutokana na bidhaa zinazoletwa na kuuzwa katika masoko na magulio yanayomilikiwa na Halmashauri;

"vizimba" maana yake ni vibanda vidogo vidogo vilivyojengwa ndani ya eneo la soko au vibanda vinavyohamishika ambavyo vimewekwa ndani ya eneo la soko kuzunguka soko mfano vibanda vya makampuni ya simu, na vingine vinavyouza bidhaa mbalimbali;

"Wakala" maana yake ni mtu, Shirika, Kampuni, Taasisi au Asasi yoyote iliyoingia mkataba na Halmashauri kwa ajili ya kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri.

## SEHEMU YA PILI
## ADA NA USHURU

Ada na ushuru

3.-(1) Halmashauri itatoza ada na ushuru kwa ajili ya vibali, leseni na huduma mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii.

(2) Ada na ushuru zinazotozwa chini ya Sheria Ndogo hii zitatakiwa kulipwa kabla au wakati wa huduma kutolewa.

(3) Ushuru utakaotozwa utalipwa kwa Halmashauri au Wakala aliyeteuliwa na Halmashauri kwa ajili ya kukusanya ushuru husika.

(4) Malipo ya ada na ushuru yatafanyika kwa stakabadhi ya kielektroniki.

## SEHEMU YA TATU
## ADA YA VIBALI VYA UJENZI

Vibali vya ujenzi

4.-(1) Kila mtu, taasisi, kikundi, Kampuni yoyote chini ya Sheria Ndogo hii pamoja na Sheria na Kanuni zinazosimamia ujenzi mijini kabla ya kuanza ujenzi wa aina yoyote ile itakuwa na wajibu kuomba kibali cha ujenzi kwa Halmashauri na kulipa ada kabla ya kuanza ujenzi husika.

(2) Kibali cha ujenzi kitatolewa baada ya mwombaji kutimiza masuala yafuatayo:

(a) awe amewasilisha michoro ya ramani ya jingo;

(b) awe amelipa ada ya ukaguzi wa ramani;

(c) awe na kiwanja au eneo linalotambulika linalokusudiwa kujengwa jengo husika; na

(d) awe amelipa ada ya ardhi kwa kiwanja kilichopimwa.

(3) Ramani zitakazowasilishwa Halmashauri zitatakiwa kuwa na vipimo vitakavyokubaliwa na Afisa Mwidhiniwa.

(4) Kibali kitatolewa baada ya mwombaji kutimiza masharti yaliyotajwa katika Sheria Ndogo hizi na baada ya kukaguliwa na kupitishwa na Afisa Ardhi, Mhandisi wa Ujenzi, Afisa Afya na Afisa Mipango Miji.

## SEHEMU YA NNE
## ADA YA UKAGUZI WA NYAMA

Ada ya ukaguzi wa nyama

5.-(1) Kila mnyama atakayechinjwa kwenye machinjio au eneo lingine lililoruhusiwa ndani ya Halmashauri atapaswa kulipiwa ada ya ukaguzi wa

nyama.

(2) Mtu yeyote hataruhusiwa kuuza, kugawa au kusambaza nyama kwa ajili ya matumizi ya binadamu kabla ya kukaguliwa.

SEHEMU YA TANO
USHURU WA SOKO LA WANYAMA

Ushuru wa soko la wanyama

6. Halmashauri itatoza ushuru wa soko kwa kila mnyama atakayeuzwa au kununuliwa katika soko la wanyama, mnadani au gulioni;

SURA YA SITA
USHURU WA MAZAO YA BIASHARA NA MISITU

Halmashauri kutoza Ushuru wa Mazao.

7.-(1) Halmashauri itatoza ushuru wa mazao kwa mazao yote ya biashara, chakula na misitu yatakayozalishwa ndani ya eneo la Halmashauri.

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1), Halmashauri itatoza ushuru kwa mazao yote yatakayoingizwa ndani ya eneo la Halmashauri kutoka eneo lingine kama ikithibitika kuwa hayajatozwa ushuru wa mazao huko yalipotoka.

(3) Ushuru wa mazao utatozwa kutoka kwa kila mnunuzi kwa kiwango kilichoainishwa katika Sheria Ndogo hii ya bei ya kununulia zao husika.

(4) Mnunuzi au mtu mwingine yeyote atakayesafirisha mazao yake nje ya eneo la Halmashauri atawajibika kulipa ushuru.

(5) Kila mnunuzi wa mazao atatakiwa kujisajili kwa ajili ya kununua mazao ndani ya Halmashauri, na baada ya usajili atapewa kibali cha maandishi cha kununua mazao hayo.

(6) Kibali kitakachotolewa chini ya kifungu kidogo cha (5) kitaonyesha-

(a) jina la zao husika;
(b) kiasi cha mazao na aina ya mazao;
(c) kiasi cha ushuru utakaotozwa kwa ajili ya mazao yanayoombewa kibali; na
(d) eneo ambapo mazao hayo yatanunuliwa.

(7) Halmashauri inaweza kukataa kutoa kibali kwa mnunuzi yeyote ambaye anadaiwa ushuru wa mazao

au ushuru mwingine wowote kwa kukiuka masharti ya Sheria Ndogo hii hataruhusiwa-

(8) Mnunuzi yeyote chini ya Sheria Ndogo hii;-

(a) kununua au kusafirisha mazao bila kibali cha Halmashauri;

(b) kununua mazao shambani kabla hajavunwa;

(c) kusafirisha mazao bila kulipa ushuru; na

(d) kununua mazao nje ya eneo lililotengwa kwa ajili ya kuuza na kununulia mazao.

(9) Mnunuzi yeyote atawajibika kutoa taarifa sahihi ya mazao aliyonunua na kuonyesha risiti aliyolipia ushuru pamoja na kibali cha kununulia mazao atakapotakiwa kufanya hivyo.

(10) Halmashauri itakuwa na uwezo wa kukamata na kushikilia mazao yaliyonunuliwa kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hii kwa muda wa siku saba (7) kwa mazao ambayo hayaharibiki kwa haraka na siku tatu kwa mazao yanayoharibika kwa haraka.

(11) Endapo mmiliki hatakomboa mazao yake baada ya siku zilizotajwa katika kifungu cha 7(10), Halmashauri itaomba kibali cha Mahakama ili kuuza mazao hayo kwa njia ya mnada.

(12) Endapo mazao hayo yatauzwa kwa mnada, Halmashauri itakata fedha inazodai na gharama za kukamata, ulinzi na kuhifadhi mazao hayo na salio litakalobaki atapewa mmiliki wa mazao hayo.

Muda wa kusafirisha mazao

8. Mtu yeyote, kikundi cha watu, kampuni au taasisi kusafirisha mazao kuanzia saa 1:00 jioni hadi saa 12:00 asubuhi.

## SURA YA SABA
## USHURU WA MADINI YA UJENZI

Ushuru wa madini ya ujenzi

9 Halmashauri itatoza ushuru wa madini ya ujenzi kwa viwango vilivyoanishwa katika Sheria Ndogo hii.

*Tangazo la Serikali Na. 217 (Linaendelea.)*

## SEHEMU YA NANE
## MAKOSA NA ADHABU

Halmashauri kuwajibika namapungufu yake

10. Halmashauri inaweza kuwajibishwa kwa kulipa hasara itakayosabishwa na Afisa Mwidhiniwa au Afisa yeyote ama kwa uzembe wake au kwa makusudi wakati wa kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria Ndogo hii.

Makosa

11. Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote chini ya Sheria Ndogo hii;-

(a) kukataa au kukwepa kulipa ada au ushuru;
(b) kushawishi mtu au kikundi cha watu kutolipa ushuru;
(c) kumzuia au kujaribu kumzuia Afisa Mwidhiniwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;
(d) kujenga jengo lolote bila kibali cha ujenzi;
(e) kuchinja mifugo bila kukaguliwa;
(f) kufanya matangazo bila kuwa na kibali;
(g) kuendesha gari kwa madhumuni ya biashara bila kuwa na lessen ya biashara kutoka Halmashauri; na
(h) kuegesha gari katika maeneo yasiyoruhusiwa.

Adhabu

12 Mtu yeyote ambaye atatenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hii atakuwa ametenda kosa, na atakapotiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua laki mbili na isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au vyote viwili kwa pamoja.

Kufifilisha kosa

13 Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kiasi cha shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

*Tangazo la Serikali Na. 217 (Linaendelea.)*

JEDWALI LA KWANZA

Limetungwa chini ya kifungu cha 3(1))

(a) ADA NA USHURU WA MAZAO YA MALIASILI.

| Na. | AINA YA ZAO | KIWANGO CHA USHURU NA ADA |
|---|---|---|
| | Kibali cha kuvuna mti/miti | 2000/= kwa kila mti |
| | Ada na ushuru wa uanzishwaji na Uendeshaji wa Bustani za Miti | 10,000/=kwa mwaka |

(b) USHURU WA KUEGESHA MAGARI YANAYOINGIA KATIKA MAGULIO, MASOKO NA MINADA.

| Na. | AINA YA GARI | USHURU KWA SIKU |
|---|---|---|
| 1. | Gari au basi kubwa | 2000/= |
| 2. | Magari madogo (hiace) | 1000/= |
| 3. | Taxi | 1000/= |
| 4. | Bajaji | 500/= |
| 5. | Pikipiki | 200/= |
| 6. | Gari dogo la mizigo (lori au pick up). | 2000/= |
| 7. | Magari binafsi yasiyo ya biashara chini ya tani 7 | 500/= |
| 8. | Gari kubwa la mizigo zaidi ya tani 7 | 3000/= |

c) ADA YA UKAGUZI WA NYAMA

| Na. | Aina ya Mnyama | Kiwango cha Tozo | Idadi |
|---|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | 3000/= | - Kwa kila Ng'ombe |
| 2. | Mbuzi | 1000/= | - Kwa kila Mbuzi au Kondoo |
| 3. | Kondoo | 2000/= | - Kwa kila atakayechinjwa |
| 4. | Nguruwe | 2000/= | - Kwa kila atakayechinjwa |

d) USHURU WA SOKO LA NGOZI

| Na. | Aina ya Mnyama | Kiwango cha Tozo | Idadi |
|---|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | 300/= | Kwa kila moja |
| 2. | Mbuzi | 200/= | Kwa kila moja |
| 3. | Kondoo | 200/= | Kwa kila moja |

*Tangazo la Serikali Na. 217 (Linaendelea.)*

e) ADA YA VIBALI MBALIMBALI

| Na. | Aina ya Kibali | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Kukodi gari dogo | - Tshs 1,600/= kwa kila kilomita moja. |
| 2. | Kukodi Lori. | - Tshs. 250,000= kwa saa nane. |
| 3. | Kukodi viti | - Kwa mujibu wa mkataba |
| 4. | Kibali cha kukodi ukumbi wa Halmashauri kwaajili ya semina au sherehe. | - Kwa mujibu wa mkataba |

f) ADA ZA BURUDANI

| | AINA YA BURUDANI NA UTAMADUNI | ADA NA USHURU WA KIBALI |
|---|---|---|
| 1. | Muziki (disko, dansi na Taarabu) | 50,000/= kwa tukio |
| 2. | Burudani msanii binafsi | 50,000/= kwa tukio |
| 3. | Maigizo ya mazingaombwe | 10,000/= kwa tukio |
| 4. | Kuonyesha video/Runinga au sinema au Mpira | 60,000/= kwa mwaka |
| 5. | Leseni ndogo kwa waganga wa kienyeji | 100,000/= kwa mwaka |
| 6. | Matangazo au Promosheni | 50,000/= kwa tukio |
| 7. | Mashindano ya urembo (Miss) | 50,000/= kwa tukio |
| 8. | Mchezo wa pull(Pool Table) | 40,000 /= kwa mwaka |
| 9. | Wamiliki wa kumbi za burudani | 100,000/= kwa mwaka |
| 10. | Kupiga picha za video | 20,000/= kwa tukio |
| 11. | Burudani nyinginezo | 50,000/= kwa tukio |
| 12. | Usajili wa vikundi vya sanaa | 60,000/= kwa kikundi |
| 13. | Usajili wa vyama vya michezo | 30,000/= kwa mwaka |
| 14. | Michezo ya bahati nasibu | 100,000/=kwa mwezi |
| 15. | Mapromota | 200,000/= kwa mwaka |

g) ADA/ KIBALI CHA UJENZI

| Na. | AINA YA JENGO | ADA (Tshs.) |
|---|---|---|
| 1. | Ghorofa | 250,000/= |
| 2. | Jengo la Makazi | 30, 000/= |
| 3. | Jengo la Makazi na biashara | 50, 000/= |
| 4. | Mnara | 300, 000/= |
| 5. | Kituo cha mafuta na huduma | 200, 000/= |
| 6. | Shule binafsi, na Hospitali binafsi | 100, 000/= |
| 7. | Ofisi binafsi | 100, 000/= |
| 8. | Magahala au mabohari, makarakana | 100,000 |
| 9. | Uzio wa ujenzi | 50,000 |
| 10. | Kiwanda | 100,000 |
| 11. | Majengo mengine ambayo hayajatajwa | 30,000 |

*Tangazo la Serikali Na. 217 (Linaendelea.)*

h) ADA YA MABADILIKO YA JENGO LILILOPO

| | AINA YA JENGO | KIASI (SHILINGI) |
|---|---|---|
| | Nyumba ya kuishi | 10,000/= |
| | Nyumba ya biashara | 15,000/= |
| | Ghorofa | 100,000/= |
| | Kiwanda, bohari, ghala, n.k | 100,000/= |
| | Majengo mengine ambayo hayajatajwa | 20,000/= |

i) ADA YA KUOMBA ZABUNI

| | AINA YA ZABUNI | KIASI CHA ADA |
|---|---|---|
| 1 | Uwakala | 50,000/= |
| 2 | Zabuni zingine | 100,000/= |

j) USHURU WA KITUO CHA MABASI YA ABIRIA

| | IDADI YA ABIRIA | KIWANGO CHA USHURU KWA SIKU |
|---|---|---|
| 1 | 4 – 9 | 1,000/= |
| 2 | 10 – 25 | 1,500/= |
| 3 | 26 – 35 | 2,000/= |
| 4 | 36 – 65 | 3,000/= |
| 5 | 66 au zaidi | 5,000/= |

k) USHURU WA KUEGESHA MAGARI YA MIZIGO

| | Uzito wa gari | Kiwango cha ushuru kwa siku |
|---|---|---|
| 1 | Chini ya tani3 | 1,000/= |
| 2 | Tani 3-6 | 2,000/= |
| 3 | Tani 7-10 | 3,000/= |
| 4 | Zaidi ya tani10 | 5,000/= |

l) USHURU WA MIFUGO MINADANI

| | AINA YA MIFUGO | KIWANGO CHA USHURU |
|---|---|---|
| 1 | Ng'ombe | 4,000/= |
| 2 | Mbuzi | 1,000/= |
| 3 | Kondoo | 1,000/= |
| 4 | Kuku/Bata | 200/= |
| 5 | Punda | 3000/= |

m) USHURU WA MADINI YA UJENZI (MAWE, MCHANGA, KOKOTO NA MATOFALI)

| Na | Aina ya madini | ujazo | Kiwango |
|---|---|---|---|
| 1. | Changarawe tani 1 | Tripu moja | Tsh. 500/- |
| 2. | Udongo( Claysoil) kwa ajili ya kutengeneza "Slavy" ya kutengeneza saruji au shughuli yoyote tani 1 | Tripu moja | Tsh. 500/- |

*Tangazo la Serikali Na. 217 (Linaendelea.)*

| | | | |
|---|---|---|---|
| 3. | Kokoto tani 1 | Tripu moja | Tsh 500/- |
| 4. | Mawe tani 1 | Tripu moja | Tsh1,000/- |
| 5. | Udongo kwaajili ya kutengeneza tofari tani 1 | Tripu moja | Tsh. 500/- |

n) USHURU WA MAZAO YA MISITU

| Na | Aina ya za | Ushuru (TShs.) |
|---|---|---|
| 1. | Mbao za aina zote na saizi zote ujazo wa $m^3$ | 5% ya bei ya kununulia |
| 2. | Nguzo miti laini ujazo wa $m^3$ | 5% ya bei ya kununulia |
| 3. | Nguzo miti migumu /asili ujazo wa $m^3$ | 5% ya bei ya kununulia |
| 4. | Nguzo mzigo ujazo wa $m^3$ | 5% ya bei ya kununulia |
| 5. | Kuni kwa mzigo ujazo wa $m^3$ | 5% ya bei ya kununulia |
| 6. | Kuni kwa ujazo wa $m^3$ | 5% ya bei ya kununulia |
| 7. | Mkaa ujazo wa $m^3$ | 5% ya bei ya kununulia |
| 8. | Miche ya miti ya kawaida ujazo wa $m^3$ | 5% ya bei ya kununulia |
| 9. | Miche ya miti ya matunda na mapambo ujazo wa m3 | 5% ya bei ya kununulia |
| 10. | Viwanda vya useremala | 20,000/=kwa mwaka |
| 11. | Nyungo | 5% ya bei ya kununulia |
| 12. | Mikeka | 5% ya bei ya kununulia |
| 13. | Vinu – kidogo | 5% ya bei ya kununulia |
| 14. | Vinu – kikubwa | 5% ya bei ya kununulia |
| 15. | Pinde | 5% ya bei ya kununulia |
| 16. | Fagio | 5% ya bei ya kununulia |
| 17. | Kamba | 5% ya bei ya kununulia |
| 18. | Asali | 5% ya bei ya kununulia |
| 19. | Ushuru wa pumba za kuchomea tofali ujazo wa $m^3$ | 5% ya bei ya kununulia |

o) USHURU WA MAZAO

| Na. | Aina ya mazao | Kiwango cha ushuru |
|---|---|---|
| 1. | Mazao ya biashara | 3% ya bei ya kununulia shambani |
| 2. | Mazao ya chakula | 3% ya bei ya kununulia shambani |

p) ADA YA USAJILI WA VYOMBO VYA UVUVI

| | *AINA YA ADA* | *KIASI KATIKA SHILINGI* |
|---|---|---|
| 1 | Kusajiliwa kwa chombo cha uvuvi | 10,000/= kwa mwaka |
| 2 | Leseni ya chombo cha uvuvi | 15,000/= kwa mwaka |
| 3 | Leseni ya uvuvi | 15,000/= kwa mwaka |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 13)*

HATI YA KUFIFILISHA KOSA

Mimi.........................................................................................nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya ............................................................. ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi kwamba tarehe ..................... ya mwezi ....................... mwaka ........................... nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha ................................ cha Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi ya mwaka 2022.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, nipo tayari kulipa kiasi cha shilingi laki mbili na kutimiza wajibu wangu chini ya Sheria Ndogo hiyo badala ya kushtakiwa Mahakamani.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU.

Leo tarehe.....................ya mwezi.........................mwaka......................................

Jina.................................................... Saini...........................................................

Mbele ya:

Jina:................................................Cheo:............................................

Saini.........................................................................................................

*Tangazo la Serikali Na. 217 (Linaendelea.)*

Nembo na muhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya IKUNGI umebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa Azimio lililopitishwa na mkutano wa Baraza la madiwani ulioitishwa Tarehe 22/1/2021 na ubandikwaji huo kushuhudiwa na:-

JUSTICE L. KIJAZI,
*Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya ,*
*Wilaya ya Ikungi*

ALLY J. MWANGA,
*Mwenyekiti Halmashauri ya*
*Wilaya ya IKUNGI*

L.S

NAKUBALI,

Dodoma,
9 Machi, 2022

UMMY A MWALIMU
*Waziri wa Nchi-OR-TAMISEMI*